

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 02 mwezi 05 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VEIN KAGERA, S.L.P. 906,  
BYKOSA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana  
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

ZAKAYO PETER KANYERERE S.L.P. 200, MAGU  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya  
KWIMBA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za  
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya KWIMBA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya  
PLASTERING & RENDERING NGUZA WIMA NA MLOO NA CANOPY  
ZAKE KWA JENGE LA KARAKANA ZA MAGARI NA YCHOMELIAI  
2400A

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo  
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 3,200,000/=, Fundi  
atafanya kazi ya PLASTERING & RENDERING kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.  
Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

**2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

**3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya gharama ya ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya gharama ya ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya gharama ya ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100:20 ya gharama ya ufundi; na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "muda wa matazamio":5 ya gharama ya Ufundi.

**4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo tarehe 02 mwezi 05' 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 24 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

**5. WAJIBU WA FUNDI**

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kutengeneza na kufunga PLASTERING na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

Jina: JULIANA NWADESA Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: KAIMU MKUU WA CHUO Tarehe: \_\_\_\_\_

Mbele ya (Shahidi)

Jina: YOHANA AZZA Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: SISE ENGINEER Tarehe: \_\_\_\_\_

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: Zakayo Peter Kanyere Mbele ya Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: \_\_\_\_\_

Mbele ya (Shahidi)

Jina: RICHARD EMMAUEL Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: FUNDI MSAUDIZI Tarehe: \_\_\_\_\_